

**DHIKI NA NGUVU YA  
WAFANYI KAZI KATIKA  
SEKTA YA JUA KALI: VISA  
VYA WANAWAKE  
WANAOFANYIA KAZI**

Feminist  
Participatory  
Action  
Research



Alice Maranga  
Nkirote Laiboni  
Pamoja Na:  
Joyce Mutoka



Federation of Women Lawyers (FIDA-Kenya)

February 2010

## UTANGULIZI

Ukuaji wa kazi nchini Kenya umechangia kwa kiasi kikubwa kupungua kwa nafasi za jamii na uchumi katika maeneo mengi ya mijini, na pia kwenye nchi za jirani kumekuwa na ongezeko kubwa la wahamiaji wanaotoka mjini kwenda vijijini na kutoka mataifa kwa miaka sasa. Ongezeko la wahamiaji kutoka mijini kwenda katika majiji na miji ya katikati ya Kenya wamekuwa hawaingii katika sekta maalumu ila hufanya kazi katika mazingira yasiyo salama na sekta isiyokuwa maalumu. Zaidi ni kwamba sheria za Kenya zimekuwa zikikataza wakimbizi kuishi katika maeneo ya mijini ndio maana wakimbizi wengi ambao wanahamia jijini na mijini wanaishia kufanya kazi katika sekta zisizo kuwa rasmi. Ingawa sekta hizi zisizo maalumu zimekuwa zikichangia ukuaji wa uchumi wa nchi bado zinaendelea kupuuzwa na watunga sera. Kwakuongezea, mchango mkubwa unaofanywa na wanawake wahamiaji umekuwa pia hautiliwi maanani. Hii inakanushwa na wanawake ambao wamekuwa wakichangia kwa kiasi kikubwa ndani ya sekta hii.

Kwa kutumia muundo wa wanaharakati wa haki za wanawake katika utafiti huu, somo hili limekuwa likieleweka kutokana na uzoefu wa wanawake waliohamia katika jiji la Kenya, Nairobi na kufanya biashara ama kupata ajira katika sekta isiyorasmi. Kwa kufanya nao mahojiano, katika mijadala ya vikundi na katika zoezi la kuchagua jamii, watafiti wameongea na wanawake katika maeneo yenye msongamano wa makazi ya watu jijini Nairobi kama Kiamaiko, Kawangware na Kangemi ili kuelewa njia walizotumia kuingia kwenye makubaliano ya maisha wanayoishi na uhalisia wake kama wanawake wahamiaji wafanyakazi katika sekta isiyorasmi. Jambo kubwa lilikua ni jinsi ya uingiaji na uzoefu wao na hali ya maisha wanayoishi na jinsi mfumo wa ujinsia unavyoeleza uzoefu wao katika soko la ajira. Maswala kama ya unyanyasaji wa kijinsia hayamo ndani ya majumba tu bali hata katika sehemu za kazi na tofauti katika uzoefu kwenye mazingira ya kazi ukilinganisha na wafanyakazi wenzao wanaume inakuja kutokana na taarifa na pale ambapo kuna matatizo makubwa ambayo wanawake wanakabiliana nayo.

Ukosefu wa maarifa ya ufanyaji biashara na pia upungufu wa mitaji ya kuanzisha na kuendeleza biashara ni kikwazo kikubwa kwa wanawake hawa. Maswala mengine ni pamoja na ukosefu wa misaada kutoka kwa waume zao majumbani na kwa wanaume wenzao serikalini. Labda kubwa gumu zaidi kwa wanawake hawa ni vikwazo wanavyowekewa na kukutana navyo kama watu wa pembezoni na wanaobaguliwa kama kukamatwa nakufirisiwa vitu(mali) vyao, kutokuwa na miundo mbinu mizuri na huduma nzuri, kutozwa ushuru mkubwa kupita kiasi, kufanyiwa ukatili wa vipigo na mapenzi na kukosa ulinzi wa kisheria na haki kutoka kwa serikali.

Mtindo wa FPAR unaunganisha vitendo na katika utafiti huu wa vitendo umefanya mtindo wa kuanzisha vikundi vya wanawake wafanyakazi katika sekta isiyokuwa rasmi ukiwa na malengo ili kupata haki katika ajira. Mchakato wa uunganishaji umekuwa ni kama njia ya mafanikio katika sekta hii kwa wafanyakazi kwa ujumla kufikia kupata haki za kikazi na hali nzuri wanazohitaji. Katika hili washiriki katika utafiti huu wameanzisha vyama vya ushirika ili kutatua matatizo wanayokumbana nayo wanawake

kazini katika sekta hii isiyo rasmi. Kwa washiriki watafiti, vyama si tu njia ya kupata haki zao ndani ya soko la ajira, bali wanasaidia kufanya njia nzuri katika kupata suluhu ya hali ya matazizo.

Umuhimu wa kusaidiwa na sera kwenye sekta isiyo rasmi serikalini na mchango wanaouonyesha wafanyakazi wanawake kwenye maisha ya uhamiaji katika sekta ni kutiliwa mkazo zaidi. Kitu muhimu zaidi cha kusisitiza ndani ya taarifa hii vilevile ni lazima kuwe na mapitio ya sera ambazo zipo tayari ili kuhakikisha kuwa si tu sekta isiyo rasmi inatambulika bali hata pia wale wanaokumbana na ubaguzi katika sekta hii wanawake na wafanyakazi wahamiaji wanalindwa na kusaidiwa. Kikubwa cha muhimu ni msaada kutoka serikalini katika kuimarisha miundombinu na kutengeneza mazingira mazuri ya kazi.

Muendelezo wa kusaidia wa mashirika yasiyo ya kiserikali kama vile GAATW na FIDA, uzoefu wa wanawake hao usiishie hapo bila ya kusikilizwa. Ni kupitia taarifa hii uzoefu wa wanawake hawa utaleta mwanga na mabadiliko yasiyo na ukomo katika maisha yao.

Taarifa hii ni mwanzo tu wa matumaini kuleta mabadiliko katika kuboresha sera ya serikali ya Kenya kwenye sekta ya kazi isiyo rasmi na imekuwa ikiathiri maisha ya wafanyakazi wote wahamiaji kwenye sekta hiyo isiyo rasmi na kuleta mabadiliko chanya katika maisha yao nchini.